

MAKAO YA KUKODI INCHINI AMERIKA

Amerika, batu mingi banapanga ao banaikala na bengine. Wakati wa kutafuta nyumba, ni vizuri kujua pesa ngapi unaweza kulipa, bei ya kawaida ya kupanga ku eneo yako, na pia mahitaji yako ya nyumba.



KUHUSU MAKAO YA KUPANGA INCHINI AMERIKA

Kuna aina nyingi za nyumba za kukodi; kuna majengo kubwa ao kidogo, ya gorofa, duplexes (nyumba mapasa), nyumba yenyi kugawanywa mu vyumba, na nyumba kwenyi unaweza kukodi chumba tu. Nyumba za kukodi, duplexes, na nyumba kawaida iko na jiko, sebuleni na eneo la kulia, chumba cha kulala, chumba cha kuoga na W.C. moja ao zaidi. Nyumba ya kukodi ya familia mingi iko na fasi za kuchangia, kama vile jiko, eneo ya kulia na mara nyingi chumba cha kuoga na W.C.



Aina ya nyumba zenye zinapatikana zinafuatana na eneo yam ji. Katika miji kubwa, mara nyingi utapata vyumba vya kukodi tu. Inje ya miji, kandokando ya miji na katika miji kidogo, utapata muchanganyiko wa vyumba na nyumba.




Wakati unakodi, unalipa bei uliyokubaliana na mwenye nyumba ao musimamizi wa nyumba kila mwezi. Mara nyingi utasinye makubaliano ya kukodi inayoitwa kontra.



Kontra inahakikisha kuwa utaikala mu ile nyumba kwa muda muliyopatana na kwa malipo muliyopatana kila mwezi.

MBELE YA KUTAFUTA NYUMBA

Fikiria mahitaji yako juu ya nyumba; mahitaji ni ile mambo ya **lazima** kwa kuishi kwa usalama na amani, hasa kama kuko mutu kilema kati yenu. Ufikirie pia kama vitu hivi viko mbali ao karibu: kwenye unatumikia, maduka ya vyakula, masomo, fasi ya ushirika, muktaba, na kituo ya autobus. Kitu cha mwisho ni kufikiria kama utapata msaada wa jamii na familia rahisi.



Hesabu ya mapato yako itakusaidia kuamua nguvu yako ya malipo ya nyumba ya kila mwezi, kwani kwa kawaida nyumba itakuwa garama kubwa kuliko zingine. Kwa kawaida, Waamerikani wanajaribu kulipa kodi ya nyumba isiyopita 30% ya mapato yao. Lakini wageni wengi wanaweza kulipa 40% ao 50% kukodi nyumba wanayohitaji.



KUPATA NYUMBA YA BEI MUZURI

Hapa Amerika, nyumba iko bei sana, hasa kwa watu wa mapato chache. Lakini kuna msaada.



Msaidizi ao kikundi cha wasaidizi wako, ao Shirika la Kuwapatia Wakimbizi Makao, ao kikundi kingine cha kukaribisha kama vile AmeriCorps wanaweza kukusaidia kupata njia ya kutafuta makao.

Cultural Orientation Resource Exchange

For more information, visit Settle In at settlein.us.org.